



Hapo zamani za kale,  
kulikuwa na familia  
moja iliyoishi kwa  
amani.

Heri, Amani na Musa  
waliwasaidia wazazi  
nyumbani na  
shambani.





Wazazi wao  
hawakuwaruhusu  
waende karibu na  
moto, wala kukaa  
juani.



Heri, Amani na Musa  
walifanya kazi zao zote  
usiku.

Hii ni kwa sababu  
watoto hao  
waliumbwa kwa nta.



Musa alitamani  
kwenda nje wakati wa  
mchana.



Siku moja tamaa  
ilimzidi. Nduguze, Heri  
na Amani,  
walimwonya asiende  
juani. Musa  
hakuwasikiza.




Joto lilipokuwa kali,  
Musa aliyeyuka.



Heri na Amani  
walihuzunika  
walipomwona Musa  
akiyeyuka.



Heri na Amani  
waliichukua nta  
iliyoyeyuka  
wakamtengeneza  
ndege.



Kisha walimweka  
ndege huyo juu ya  
mlima mrefu.



Jua lilipochomoza,  
ndege huyo  
alipeperuka akiimba  
kwa furaha.

